

YALIYOJIRI KATIKA MKUTANO WA MKUU WA MKOA WA MWANZA NA WANANCHI WA ILEMELA KUHUSU SUALA LA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI SIKU YA TAREHE 13/09/2017:

- Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amewataka wataalamu wa ardhi wa Manispaa ya kutenda haki na kuwa waadilifu kwa wananchi wanaowahudumia huku akiasa namna ya utoaji wa majibu yanayofanywa na wataalamu hao.
- Mhe.Mkuu wa Mkoa amemtaka Mkurugenzi kukamilisha zoezi la urasimishaji kwa wakati
- Mhe Mkuu wa Mkoa amemtaka Mkurugenzi wa Manispaa kuhakikisha kuwa kero zote zilizoibuliwa zinafanyiwa kazi na taarifa ya utekelezaji inaandaliwa na kukamilika ifikapo tarehe 13/10/2017 ambapo itawasilishwa katika Mkutano. Halikadhalika ameagiza kero zote zinazohitaji ufumbuzi wa haraka zianze kufanyiwa kazi kmara moja.
- Mhe Mkuu wa Mkoa ameelekeza kuwa yatafutwe maeneo ya kupima viwanja kwa ajili ya kulipa madeni ya fidia.
- Kuhusu suala la fidia Mhe Mkuu wa Mkoa ameagiza fidia ilipwe kwenye maeneo ya wananchi yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya umma kama vile maeneo ya shule, hospitali, maeneo ya wazi n.k
- Mhe.Mkuu Mkoa ameagiza kuwa kuwepo na utaratibu wa kufanya mikutano kama hii kwa ajili ya kutatua kero za ardhi katika kata zote.
- Kuhusiana na migogoro ya mipaka kati ya wananchi na jeshi Mhe Mkuu wa Mkoa aliahidi kuwa ataenda yeye kutembelea maeneo hayo akiwa na uongozi wa jeshi kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Mhe.Mkuu wa Mkoa ameyasema hayo wakati wa ziara ya kikazi katika Manispaa ya Ilemela kwa lengo la kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali za ardhi zinazowakabili wananchi wa Wilaya ya Ilemela ikiwemo migogoro ya taasisi za umma na binafsi, na huduma za kijamii

Imetolewa na

Kitengo Cha Teknolojia, Habari, Mawasiliano na Uhusiano

Halmashauri ya Manispaa -Ilemela